Due to the lack of basic needs, they are less endowed. For instance, a child born out of wedlock to a single mother, he will not be able to compete with those who have been in a fairly normal environment. So the government should set aside a project of counseling so that these people cannot be left out. They should provide guidance for them. On the same issue is respect; you find that some are not given respect by the society and therefore they feel intimidated. They should be given a sense of pride to know that they are themselves and they are part of the other family.

The single mother status should be recognised as independent. For instance, when a child of a single parent applies for something like a certificate for anything, he is asked to identify the father. The mother should be recognised as being adequate authority for the child's requirements.

Corruption in the court. We should look for an independent court whereby there is a council elected by the Parliament to punish or to judge the court's performances of the court. Also, the Law Society of Kenya, should be given the mandate to nominate judges for the approval of the Parliament.

On the youth; you find the youth are people who are very vulnerable to society in terms of corruption theft, so they should be given sometime to have what we call tax free services.

On moral values, they have said about Kithitu, but we should also have moral values governing some communities for example witchcraft. Witchcraft is always there in Kamba community. In Kisii we see they are always stoned and killed, and we see the community is not given a chance to entrench them into the Constitution. With that, thank you very much.

Com.Aroni: Asanti. John Kyule.

Mr. Kyule: Mimi yangu ni machache. Mimi naonelea katika nchi yetu ya Kenya kuna matatizo sana. Kwa hivyo, kwa maoni yangu, ningenelea kwa Constitution yetu, tusiwe na kitu kama foreign exchange. Hiyo ndio kitu ile imeleta shida sana hapa nchini kwetu, kwa hivyo utakuta watu wengi wamekuja hapa kwa sababu foreign exchange ni rahisi kuipata. Ndio wahindi wanakuja hapa usiku na mchana kutoka kwao. Kwa nchi zingine, foreign exchange ni ngumu sana kuipata. Ndio utapata lakini uta apply through Central Bank upate.

Ile nyingine ni kuhusiana na mambo ya rais asiteue mjumbe maalum au councilor maalum asiwe na hizo nguvu za kuteua na hizo nguvu. Lingine ni rais asiwe mkuu wa majeshi ya Kenya, kwa sababu yeye, huo ujuzi anaye yule mkubwa ambaye anajua mambo ya majeshi.

Lingine ni pesa za kutoka nje za msaada. Utakuta pesa zimetolewa na nchi zingine kama Saudi Arabia au mahali pengine popote, halafu hizo ni zile tunaziita za development. Hizo pesa zinaletwa kwa Treasury na utakuta kama zimeletwa kwa mradi Fulani hizo pesa zimepotea zimetoweka. Kungekuwa na kamati maalum ambayo ingeweza kusimamia pesa kama hizo kutoka nje zisiingizwe katika treasury.

Lingine ni hao watu wanaingia kutoka nje hawa foreigners wanasemekana wanaitwa ma-expatriates. Utaona tunafanyad kazi moja mimi na yeye na utakuta mshahara wake ni mkubwa kuniliko na mimi na yeye nina elimu kumliko. Sasa hii nchi yetu imetuweka nyuma sana kwa sababu ya mambo hayo. Kwa hivyo foreigner yeyote hapaswi kupewa mshahara mkubwa kuliko mkenya. Mwenye nchi apate mshahara mdogo haiwezekani hiyo pia iwekwe kwa Constitution.

Lingine ni kama mimi nimetoka cheo kikuu nimeenda kwa kampuni Fulani attachment, nitaenda nakuta mtu mwingine hana masomo na mimi nimetoka university na mimi nimepewa huyo mtu anifunze hiyo kazi, yeye kwa kweli ako na degree na yeye hana. Yule anayemfunza huyo kazi, ile akonayo ni practical lakini theory hana. Maneno hiyo inafaa kuangaliwa iwekwe katika Constitution. Tuwe watu wale wako na ujuzi na hawa elimu ya kutosha na wafikiwe.

Mambo mengine ni security. Utakuta security hapa kwetu imeenda chini kwa maana ukifika mahali kama airport utakuta mikoba ya watu wakubwa haikaguliwi na hata kama inakaguliwa inapita kwa njia zingine. Utakuta nchi zingine watu wakubwa mikoba yao hukaguliwa. Kwa hivyo ndiyo manake hata vitu zingine zinaingia hapa kwa sababu vitu vingi vyetu havikaguliwi. Kwa hivyo nayo hiyo inapaswa ikaguliwe.

Jambo lingine ni juu ya masomo. Mtu yapaswa kutoka standard one mpaka standard eight, masomo yapaswa kuwa ni free kwa sababu nchi yetu tunaamini iko na pesa. Kwa hivyo education kutoka standard one mpaka standard eight iwe ni free. Zaidi ya hapo tutajitahidi kupata hiyo mambo mengine. Asante, nitafikisha hapo.

Com.Aroni: Asante. Edward Mutisya; Joseph Ng'ang'a, James Mung'ata. Cecilia Tito, you want to speak?

Ms. Tito: I have a memorandum.

Com Aroni: So do you want to highlight or do you want to hand it over. Okay please.

Ms. Tito: I'm Cecilia Tito from Kisaingo. Mine are just on basic rights especially for women. The first basic right I would want women to be granted is land and property ownership. May any land or property of any family be equally shared between the children regardless of their sex please and let this be part of the amendment of the Constitution. Especially in Ukambani women are not supposed to own anything. I should say that as far as women are concerned in this area, no one has been issued with a title deed as one colleague said here. So I request that this should be part of the Constitution and every Kenyan child regardless of sex should have a title deed and access to the land of the family.

The other basic right I have is that women should have access to control of family resources and this is in order to make them self-reliant. Elaborating on this, may I say that a woman is not allowed to slaughter a chicken without the permission of the husband or any male in that family. Sometimes even a son is able to slaughter or sell anything but a mother cannot.

The other thing I request the Constitution to include is that wife beating should be banned completely in our country. This has made women not comfortable in their families and this has hindered development in the community.

The other thing I request the government or whoever is concerned is to ban all harmful cultural practices. These include female genital mutilation, I request that this be banned completely and any community found practicing it there should be action taken against them. The other thing I am requesting the Constitution is if for example a husband dies and this man had written a will and it doesn't favour the legal wife. I am asking, can it be revoked such that the legal wife be in custody of what belonged to this man and may it be stated that this legal wife should be the owner of everything this man had. Because sometimes we find we have a problem with these widows left behind. Can this be made legal, that the wife of this man should be the owner of everything that this man left behind.

Another thing I have as a human right regards rapists. If possible please, can the Constitution include that any man who rapes a woman and we are calling it a rape, because it was done against her will can there be something like life imprisonment or may be hanging. Those are the few points I have the rest is written.

Com. Kabira: You are talking about a legal wife are there other wives that are not legal because we would like to be very sure. You are saying the legal wife to be the one to inherit. Who's a legal wife?

Ms. Tito: A legal wife especially in Ukambani is the one who's married traditionally. May I elaborate on this, two goats and a third one have been sent to the father of this woman. The one who's traditionally married, and

she has a legal document the marriage certificate or an affidavit so that is a legal wife.

Com. Aroni: Naomi Wambua, Sammy Mutiso

Mr. Mutiso: Sina mengi, yameongewa laking nitaongezaa kidogo kwa sababu ya ukosefu wa kazi naonelea vijana wetu wapatiwe kazi ya vikundi na serikali ili wajipatie riziki, ili ujambazi na unyang'anyi upunguzike.

La pili wazee wakifikia zaidi ya miaka sitini, wapatiwe allowance na serikali ili wajisaidie kwa siku zilibakia za maisha yao.

Tatu, wale waliopigania uhuru wapewe usaidizi na serikali kwa hali na mali.

Nne. Uwezo wa rais usiwe zaidi kuliko kiasi kama ilovyokuw hapo zamani.

La tano, kwa sababu sisi ndio tuliwachagua wabunge, naonelea wafanye kazi kwa siku tano kwa wiki kwani muda wao wa kupumzika ni mwingi.

La sita, wasichana ambao hawajaolewa na wadmezalia nyumbani serikali itenge pesa ili wapatiwe kazi ya kufanya hata kama ni kwa vikundi ili wasaidie watoto wao. Itakuwa ni njia moja ya kupunguza magonjwa kama ukimwi.

Saba, machokora wahusishwe kwa ujenzi wa taifa kama, wawekwe pamoja kwa njia ya kuwa unganisha kwa kazi kama useremala, umechanic, au kazi maalum ambayo itawasaidia kupata pesa ya kuwasaidia ili wajiskie wakenya halisi.

Kiapo ya Wakamba iwekwe maanani kikatibu kwani Wakamba manaamini ndicho utambua ukweli wa mambo ulivyo.

Nane, wazee wa kijiji wawekwe maanani kikatibu kama ndio wanoweza kusikiza malalamiko kijijini kabla kufikia Assistant chief au chief. Kwa hivyo wapewe mshahara kama wafanyikazi wengine wa serikali. Asante.

Com.Aroni: Asanti. Paul Mwau. Paul Mwau.

Mr. Mwau: Asanti sana Commissioners. I've written some points in English and I'm going to read them to you. They are around ten. My recommendations.

The Constitution should be written or renewed reflecting to minimize the gap between the poor and the high

class people. I agree with the Constitution making for any society without no or Constitution is not a society not is it there.

Two, I suggested that the judiciary which is the third arm of the government should be completely independent. The executive and the legislature should not tamper with it at all.

Three, I have the view that the salaries and the benefits of the M.P's should be determined by the legislators, but it must be controlled by the economy of the country. I suggest that we remain with the unitary government for some are poorer than others to practise majimboism. Neo-colonialism should be avoided.

Next one, I have the view that the Constitution provides free education in primary, standard one to seven or eight or if the economy improves, free medical facilities. I suggest that Kenya should start diversifying and look at the possibility of mining and industrial plants to avoid relying on agriculture only.

I suggest that in the succession of the President, he or she should remain or attend the Presidential college for three months to be advised by seven or nine statesmen also handing over and taking over.

Next one, I have the view that should be owned individually, but those who do not utilize it fully should send it to the landless. Large scale farming should be to a certain limit for the landless. Owners should sell it to them willingly.

I have recommended the care of disabled for free education, basic standard one to eight and be trained the right job to make him or her earn a living.

I have just three points and then I finish. In defence, the national security in declaring war or the use of force, the President should be advised by seven to nine advisors who he/she calls to the state house time to time for advise.

Next one, Constitution supremacy should remain but should be reviewed to suit the Kenyan or citizen and reflecting to poverty reduction.

Citizenship should be regarded as a birth right. Where non-citizens break the law, they should be repatriated back to their original countries.

Last one, Taxation should be imposed without exception to make sure the needy persons are catered for. That is the end.

Com.Aroni: Asante. Philip Mbinda.

Mr. Mbinda: Asanti, wana commission na wananchi. Mimi ni Philip Mbinda. Neno yangu ya kwanza na uandike vizuri bwana D.C. President achaguliwa kutoka (?) pale. Hiyo ni maono yangu. Akiingia awe President hapana fikiria upande wa hapa, hapa, pale. Huko kuna Minister. Na kama mimi ni mzee na nina mtoto wangu wa kwanza na wa pili na wa tatu. Kila mmoja na mgawia kazi yake, na mama ndio vice. Sasa vile President na vice-President hawa ndio wenye kiti, asiteremke huko chini. Awachie watu wale wengine nafasi. Hiyo ni maoni yangu. Akae kwa Bunge kwa miaka kumi.

Kile kingine ni Bunge. Hii Bunge ilianza na hii kazi tangu marehemu Mbolu, na Kenyatta huko. na ilikuja vizuri kidogo kidogo, kuja kupitia President Moi, inakuja tena inakuja kidogo mzuri mzuri, ikipika mahali, ikaanza kuchezea kichwa ya wanadamu. Wananchi kucheza namna gani? Hii inapangwa hii kesho inageuzwa hii. Ie inapangwa ile kesho, inageuzwa hii na hiyo mimi naona ni sababu ya ile watu kidogo tuna wachagua akili zao ndogo. Hiyo akili zao bado komaa mimi naogopa hile kitu inaitwa kiapo amini ya mkamba, ninaogopa kitu ingine inasema (?) Simunajua hiyo ni mbaya lakini hao hawajui. Wanavaa viatu wanasema kama ni laana, nitaingia kwa gari haitanifuata, hiyo ndio shida ile inatusumbua. Kama mtu anachaguliwa, ajue nimechaguliwa na division Fulani na hapo ndipo mimi na kulia na akienda pale ile ka-mkate kana ng'ang'aniwa huko, akate kidogo atuletee. Hiyo ni maoni yangu.

Haya kwa elimu hapana kuchagua mjumbe mjinga, yule wa standard eight kwa sababu anajua kuzungumza vizuri sababu ukoo wao ni wa uongozi, hati anasema degree sio mbomu. Watoto tunawasomesha wa nini? Si kila mtu ako na mtoto asukuma paka apate degree, si sawa, na ni ya nini? Kuna mmoja, ana ma-degree matatu, mbili, nne na hiyo ukifuata hiyo degreee, utakuta kuna nyakati fulani na ingine ya kazi fulani. Na kama ni ingine ya agriculture, achaguliwe mjumbe si hiyo niile taabu sasa. Na hiyo, hiyo tuangaalie.

Hapa kusema ukoo fulani ama mtu Fulani anajua kuzungumza elimu ndio msingi, sababu hata anaweza kuwa President si hati yule anakuwa preasident ndio kwao kuzuri. Hata mkamba anaweza kuwa President, hata kikuyu amekuwa, hata jaluo, hata maasai, hata ile watu ako chini anaweza kuwa President. Kwa hivyo hiyo muandike vizuri hiyo mchezo ya kuchezewa hapa kifiani kwetu, wananchi hatutaki.

Kile kingine ni hii mambo ya usalama. Taabu iko na sijui kama ni taabu ya pesa sijui ni taabu gani, nikipeleka maneno yangu polisi, na hii mzuri kabisa, ile wazi kabisa naambiwa wee mzee angaia wewe pinduka pande hii, ala, kwani mimi natoka nyumbani na taabu hii yote na sina kitu sasa unaniitiza ingine. Ninaambiwa kama gari wewe apana weka mafuta wewe kwenda tu. Kwa sababu ukiwa na pesa nyingi, unakuja kunyang'nya mimi maskini. Na hii amini yetu hii, vile iliondolewa, basi matajiri umeona mwingine, alikuja akafanya kesi shamba,

sasa watoto ni kidogo, saa hile watoto wanakuja kuingia kazi wanapata pesa nyingi, haya mzee akaondosha kesi, wacha uone. Kesi inaendelea, inaendelea, mimi nataka kiapo, hakuna kiapo Kenya, mpaka sijui hao watu wameokolewa na Mungu.

Kile kingine ni hii wajane. Mimi nimeenda nikatongonza msichana na baba aliniambia wewekijana tafuta bibi. Hii mambo ya ukora ukora, mimi hapana taka. Na mimi naenda natafuta ile bibi yangu, ile msichana mzuri tunapendana, basi tukaoana. Tukakuja nyumbani. Tukaanza kuzaa mtoto wa kwanza wa pili wa tatu, wane mimi nakufa. Wacha uone wandugu sasa, hii shamba ni yetu, hii mali yetu, hawana hawa, hata hawajui Mungu anaweza kuuwa mmoja saa hiyo. Hiyo kile kitu mimi naweza kiandikwe hapo, kama ni mjane anawachwa na baba yake, kama ni mnyama mwingine anaingilia hapa na ni ndugu, sikiza, kama ni mnyama anaingilia hapa na ni ndugu, huyo afungwe miaka ishirini. Ndio wajane waone vizuri, kwa sababu, kwa nini hamukukataza hii mtoto yenu kuo. Na sasa yule anaoa, watoto ndio hawa shamba amepata, na kesho yake, mzee ameondoka, haya mali ni yetu sasa, basi, wengine wanavaa tai, wengine wana suti wengine wana magari, unaona. Andika hiyo iondelewe, miaka ishirini maoni yangu. Hiyo mnyama afungwe miaka ishirini.

Kile kingine ni hii wasichana hii, hii wasichana hii. Kuna wasichana karibu tano, na wane wameolewa, mmoja bado na, nitakuja, nimukatie shamba, nimwambie wewe kaa hapa na ujenge hapa. Haya watoto wangu wa kiume ni wanne. Saa hile mimi nitalala, wewe utatoka wewe ulikosa kuolewa, huoni hii mabibi yetu hii, sisi tumetoka kwao kwao, hii tabia yako ndio mbaya unafukuza bwana yako wewe toka uondoke, ataenda wapi? Na hiyo uandike. Kama ni msichana, anawachiwa haki yake ni, baba yake, pasiingilie mnyama mwingine hapo. Hiyo mnyama na iondelewe, kama anaingia miaka ishirini ndani andika hivyo.

Sababu shida imeingia, miaka raiia hatuna uhuru, hata mkisema iko uhuru, hakuna, ni bendera tu. Pesa zinatolewa huko, zinaiingia hapa, zinaiingia mradi fulani haya tafadhali pesa inakuja wapi? Inaibiwa huko. Sijui ni umaskini gani hii. Haya andika hivi bwana D.C. Hii party hii, imetuingiza kwa umaskini. Kama ni chama ya kparty, andika chama tatu, kwa kupigana hivi, tatu. Sababu nyumba ikiwa hapana iko bibi, hiyo siyo nyumba. Na kama ni serikali haina upinzai ina peleka sisi vile inataka. Lakini kama upinzani unateta huko unapingana huko, raia pengine wanpata nafuu kidogo. Kwa hiyo andika chama tatu hapo.

Vice President, kama huyu wetu aliteremka akakuja kugawanya mashamba, na land iko. Ile kitu ingine mimi naweza kusema, kama ni mimi mwana Kenya peke yangu, hii kasumba ya muingereza hii, ya land, ingeondolewa kabisa. Mzungu afungiwe kiombo yake, aende naye. Kama ni mashamba ikae vile tulikuwa. Niliamka nikakuta baba yangu anaweka sehemu hiyo ni ya watoto wa ng'ombe ile kidogo, baba yule mwingine huko, hii shamba ni ya kuchonga ng'ombe. Sasa hakuna ng'ombe hakuna chochote. Nje nasokotwa, paka inakuja kumalizika, sababu ya hii land hii, na ninasikia ilifanya survey ya kwetu, ninasikia ah, sisi hatutaki tuwekwe na kwa shamba moja sisi ni wa baba moja na hatutawekwa hapa. Tugawane. Tukagawane. Mimi

iko na watoto watatu, yule ndugu yuko na watoto watatu. Si hiyo sehemu yake tena ni nini hiyo tangi. Sasa hiyo, kama ni mimi mzungu, na makonge yake ameleta huku, angeondolewa naye. Sababu sasa mweupe ameondoka, mweusi ndio hodari, hata angalau wakati tulikuwa tukipatiwa unga huko kwa makonge huko. Sasa ni wangapi, ukifika hapa, toa kitu, ukifika hapa toa kitu. Sasa hii kitu, utatoa wapi, basi kwa hiyo, sitasumbua nyingi sana wacha tupike hapo. Asante

Com Aroni: Musau Kimonye.

Mr. Kimonye: (kikamba)

Translator: Katiba ama sheria ndiyo msingi wa maisha ya kukaa na watu. Sheria ndiyo yafunga mtu akifanya makosa na ndiyo inafunza binadamu. Leo nimesoma Bibilia, tunaambiwa kwa sababu ya ubaya kuenea, upendo umekwisha. Wakati wa ukoloni watu walikuwa wakiogopa sheria, kwa sababu walikuwa wajinga. Ukipatikana na makosa ulikuwa unafungwa. Na leo watu wamedharau sheria, kwa sababu ya uerevu umekuwa mwingi. Kwa sababu wale wanatengeneza bomu sio wajinga, na wale wanapindua serikali si wajinga. Leo nasema serikali ambayo iko, iangalie watu wote, wale wajinga hata wale werevu, iwaangalie kwa sababu mjinga hawezi tengeneza bomu, lakini mwerevu aweza. Kitabu cha Danieli kinasema, uerevu utazidi na ubaya utazidi pia. Serikali iendeleo kusaidia wazee ndio watu wengi wasizidi kutengeneza bomu. Kwa sababu ujuzi ikikuwa mwingi, watoto wetu pia watatengeneza bomu, na inaweza kutuumiza. Serikali iwe macho zaidi. Asante.

Com Aroni: John Mbondo. Raphael Kisuka, Ezekiel Musyoki, Peter Sukali, Mary Maithia.

Ms. Maithia: Kwa majina mimi naitwa Mary Maithia, na ningependa kidogo kuchangia kuhusu urekebishaji wa Katiba. Na ingawaje ile mambo nilikuwa nataka kuchangia, imezungumzwa na watu wachache, pia nitaongezea. Kwanza, ningetaka kuzungumza juu ya haki zetu sisi akina mama, kwa sababu sisi akina mama saa zingine hatuna haki, kwa nchi hii.

Kwa sababu ukiingia kwa mashamba, utakuta title deed ni ya baba peke yake, huwezi kuta akina mama wako na hako yao. Pamoja na kupewa ardhi kwa baba yako, unaweza kupewa ndio. Na hata saa zingine unaweza kosa kupewa kwa sababu, umeolewa na saa ingine mtu akiolewa, unaweza kuwachana na hiyo mtu. Saa zingine kunaweza kuwa na separation ama divorce. Mama anaenda wapi? Ile Katiba inasimamia mama anaenda wapi? Na pahali pa mama ni wapi tuseme kama kwa baba hakuna na kwa bwana hakuna. Saa ingine unaenda bila kujua mahali unaenda. Na saa ingine utakuwa na hao watoto na hujiue mahali utaweka. Hiyo ndiyo nilikuwa nataka nichangie.

Jambo la pili, nilikuwa nataka niongee kama mambo matatu hivi. Jambo la pili ni tuseme juu ya. Si ya pili lakini

ni kuongea tu juu ya kina mama. Mimi nawakilisha group ingine ya akina mama. Iko shida ile naona ya viongozi, haswa kina mama. Saa ingine unaweza kuwa umechagua kiongozi na hata sio anaongoza group. Saa ingine iko machairlady wale wa maendeleo. Iko mambo ingine kina mama wanaongoza bila mshahara. Ndio nimeona ile shida nyingi inapata group kupotea.

Unaona waanzisha group mara moja, halafu wanaendela halafu inaisha kwa sababu kama ni kiongozi hapati chochote, ni kuenda unakalisha watu chini, halafu mnaweza kaa hata masaa kumi hakuna kitu unapata na mnaachana.

Kwa hivyo, ningependekeza kama sisi akina mama, kwa sababu ndio tunajukumu kubwa katika jamii kafikiriwa tuone kama tukiwa mtu akishikilia pahali Fulani kwa kuongoza anapewa kiasi fulani ya pesa ya serikali kama usaidizi wowote, na tukiwa kwa hiyo kikundi, ndiyo vikundi view havivunjiki ovyo ovyo. Tunaweza kuwa tunafikiriwa zaidi kwa, kama tunapewa mshahara fulani ili tuzidi kuungana. Kama kuko na hiyo sheria nafikiri vikundi haviwezi kuvunjika ovyo ovyo. Vinaweza kuendelea.

Ile ingine ya tatu, ni mambo ya walemavu, kwa sababu hata mimi naishi kwa town fulani, naona wanashida nyingi, mwingine tuseme hata si mkamba kama mimi ati ataelewa lugha, mwingine anasungumza na mkono ati anataka usaidizi. Mtu hana macho na hana chakula ni mpaka aombe. Lakini kama kungekuwa na hiyo sheria ya kusaidia walemavu, tuseme kama mwisho wa mwezi iko kiwango fulani ile inapangiwa na hao walemavu, my anaenda anachukua kila mwezi. Na kama sio hiyo, wao wanaangalia mtaa, tuseme kama chiefs na macouncillors wapewe jukumu ya kuangalia hawa ndio wawe wanaridhika kama sisi kwa sababu hawajiwezi.

Lile lingine na nila mwisho ni la kuhusu serikali za mtaa. Tuseme kama Mayor, mimi naonelea, asiye anatoka kati ya macounnallors. Mtu awe meajiliwa. Kwa sababu alitoka katika councilors anaweza kufanya mambo akiharakiswa kwa sababu ili wakati yake ikiisha atatoka. Kama ako na hukumu ya kuuza ploti Kama ni 1town, anuza haraka haraka ile ndiye wakati yake ikiisha anaacha hiyo iko na shida. Na kama ni mtu ameandikwa, atachunga kazi kwa sababu ziko sheria zile zaweza kumpata akitoka.

Kwa hayo uashukuru.

Com. Aroni: Pauline Mbola, Alice Mutunge.

Ms. Mutunge: Mimi kwa majina naitwa Alice Mutunge na mimi ni mchunganji. Niko na umri wa miaka 65 ningetaka kuchangia kidogo na nimapendekezo tu yangu, vile mimi nimeinelea nikiwa mama mzee. Nimeandika tu pointi moja moja nikiruka ruka kwa hivyo mtanivumilia mtajua vile mtafanya kulingana na mipango yenu.

Jambo la kwanza nimezungumza juu ya ubaba, wenyeji, mwanakenya. Kwa upande wangu nimeonelea kuwa baba ndiye kichwa cha boma. Kwa hivyo mahali popote ambapo baba amesaa mtoto, huyo mtoto basi ni wa hapo. Kama mzee mwanakenya amesaa mtoto wake basi nikaona mtoto ni mwanakenya. Ikiwa babake ni mwana Kenya, si mtoto pia ni mwanakenya kwa maana kulingana na Bibilia, mwanamme ndiye kichwa cha boma.

Nikaona ya kwamba, katika mambo ya uchaguzi, wananchi wapewe uhuru wa kuchagua. Wachague yule mtu ambaye wanaona. Yule kiongozi ambaye wanapendelea. Wamchague. Na tena uchaguzi uwe wa kisiri. Usiwe ule wa mlolongo. Mlolongo utupiliwe mbali na watu wawe wakifanya uchaguzi kupitia “secret ballot” ndio mwanachi awe na uhuru wa kuchagua yule kiongozi ambaye anataka.

Haya nikatoka hapo nikaenda mambo ya, ningetaka watu wawe na uhuru juu ya kuabudu. Uhuru wa kuabudu. Wanapoabudu Mungu wao, wapewe uhuru. Aabudu Mungu wake vile anapendelea, maana kuabudu Mungu ni kuabudu yule ambaye aliye kuumba. Kwa hivyo, nikaonelea hakuitaji kuwe na kipimo. Nipimiwe vile nitaabudu Mungu aliye niumba. Nikaona kukiwa na uhuru wa kuabudu, liakuwa ni jambo nzuri. Na nikaendelea nikaona ya kwamba, ninaenda nikirukaruka kwa hivyo mtanivumilia,

Nikaenda jambo lingine juu ya wazee wa vijiji. Nikaona wazee wa vijiji wanafanya kazi ngumu sana. Akiamka anapewa kesi. Anaamua kesi mingi. Siku hiyo haendi shambani. Kwa hivyo nikaonelea, wanafanya kazi mingi ya bure. Wangepewa malipo na serikali.

Haya, pointi ingine ni juu ya madawa ya kulevya na bangi na pombe. Nikaonelea, serikali ingetia maanani sana Katiba, ione vile inaweza kupunguza haya mambo. Maana ulevi ukiendelea vile inavyo endelea, na uvutaji wa bangi, na madawa ya kulevya, hatutakuwa na taifa la Kenya kesho. Litamalizika kwa sababu ya huo ulevi. Kwa hivyo, nikaona ni jambo nzuri. Kama serikali ingekubaliana kuweka kwa Katiba kujaribu sana kupunguza mambo ya ulevi na madawa ya kulevya na uvutaji wa bangi.

Jambo lingine ni hongo. TTKK imefanyilia watu sana. Nikaonelea, mambo ya hongo, Katiba ingejalibu kupunguza sana, maana wasafili wanashindwa kusafiri. Ukifika pale, TTKK, kufika Nairobi TTKK zinakuwa ishirini. Na kurudi ni ishirini. Kwa hivyo, mwenye matatu amefanya TTKK hajapata kitu. Kwa hivyo, Katiba ingechunguza sana kujaribu kupunguza mambo ya TTKK. Jambo lingine juu ya vikongwe na mayatima na wajane na wasiojiweza. Nikaonelea ya kwamba vikongwe, na mayatima, wajane na wasiojiweza wangetafutiwa msaada na serikali maana ulimwengu huu tulio nao ni ulimwengu wa kushangaza maana wajane wamekuwa wengi sana, na mayatima wamekuwa wengi sana. Ukijaribu kuhesabu hata kijijini kwenu, utaona vikongwe, mayatima, wajane ndio wengi na wasiojiweza. Wakiwachiliwa hivyo wataangamia. Kwa hivyo nikaona kama Katiba ikiwekwa vizuri na hawa watu walindwe vizuri inaweza kuwa ni jambo nzuri.

Jambo lingine, kuna taifa la chokora. Nimekuwa nikishughulika na mambo ya chokora kule Nairobi, na nikaona limekuwa taifa nzima. Maana kuna msichana aliyeenda chokora, kijana chokora wameona, wakazaa kachokora kengine. Sasa si hilo limekuwa taifa? Nikaona kama serikali ingejaribu sana na iwekwe ndani ya Katiba, hawa chokora waangaliwe vile wanaweza kuangaliwa na serikali kama ni kupatiwa mashamba, kama ni kufundishwa ukulima, na mambo mengine, waweze kufaidika, waweze kukaa kama vile binadamu wengine wanavyoishi. Wakipatiwa mashamba na mambo mengine kama yale.

Haya, juu ya mambo ya biashara na mashamba kwa wanakenya. Nikaonelea ya kwamba lunaweza kuwa jambo nzuri mwanakenya anunue shamba mahali popote maana ni mwanakenya. Afanye biashara mahali popote maana yeye ni mwamakenya. Bila kuambiwa juu ya majimbo. Mwanakenya afanye biashara na anunue shamba mahali popote anapopata nafasi maana yeye ni mwanakenya.

Elimu ya primary school ningependelea, kama kunawezekana – maana katika nchi yetu ya Kenya kumekuwa na umaskini mwingi sana, kama nilivyotaja mayatima na wajane, na wake na watoto, hawana mapato – kama serikali ingekubali, kuwa na elimu ya bure primary school. Ili kila mtoto aonekane amesaidiwa na serikali mpaka form IV. Maana hiyo form IV atapata tu elimu tu ya kuomba maji, ya kujua njia, ya kujua ni mahali gani pako na hatari aweze kujilinda na pengine awezea kujua vipimo vya dawa wakati anapanda mboga. Kwa hivyo, nikaonelea, kama serikali ingekubaliana, kuwe na elimu ya bure ya primary school inaweza kuwa ni vizuri.

Jambo lingine ni juu ya wamama na watoto. Walindwe na serikali kuhusu unajisi. Wamama wamekuwa wakinajisiwa sana na watoto. Na mimi nimeomelea ya kwamba ingekuwa kwa Katiba wamama walindwe. Maana wamama wamekuwa wakitumiwa kwa njia mbaya na watoto. Sana sana siku hizi ambazo ugonjwa wa ukimwi umeingia, watu wengi waneapatwa na ukimwi na wakaamua kuambukiza kila wanaekutana naye njiani. Kwa hivyo wanawashika wamama, wanawa rape wanawaambukiza hayo magonjwa. Kwa hivyo mimi nikaonelea ya kwamba mtu yeyote atakayekuwa akicommit jambo kama hili, inapasa achukuliwe hatua kali ili wamama na watoto walindwe kuhusu mambo ya unajisi. Lile lingine ni juu ya bunduki. Mimi nikaonelea kwa upande wangu ingekuwa ni vizuri bunduki zisipeanwe ovyo ovyo, lakini zipaenwe kwa yule mtu ambaye anahitaji kukaa na bunduki. Kama ni MP, anajilinda kwa hatari, ama ni watu wengine kama viongozi wa serikali lakini bunduki zisipeanwe ovyo ovyo kwa kila mtu maana zikipeanwa ovyo ovyo uuwaji utazidi kuwa mwingi na nchi yetu itakuwa taabani. Kwa hayo machache nasema ahsante. Mbarikiwe.

Com. Aroni: Asante Alex Sioma

Mr. Sioma: Ahsante sana. Mimi ni Alex Sioma. Yangu ni machache, ni matatu. Kitu cha kwanza nitazungumza juu ya Bunge. Ningeonelea akiwa mtu anataka kiti cha Bunge aonyeshe assets zake kwa sababu ya kwamba

tumezidi kuwachagua waBunge ambao hawana chochote na mwishowe tutapata shida. Shida kama nini? Juzi katika Parliament, waliform commission na tukaona wamemove kutoka salary ya kshs. 70,000/= kshs.500,000/= na tukichunguza, wakenya wanazidi kutaabika wengine wakifaidika. Hatukuchagua mtu aende akafaide mwenyewe. Tulimchagua aende akazungumze masilahi ya wale ambao walimchagua. Tukirudi nyuma, tutakuta, katika every constituency, hakuna income ambayo inaweza kufikia 500,000/= ambayo wabunge wanalipiwa kwa hivyo, hasa nikionelea mimi menyewe naona iletwe watu waangaliwe katika kazi wafutwe ovyo ovyo ili mbunge apaete mshahara.Kwa hivyo tuonyeshwe mjumbe ako na mali gani akichaguliwa .Even the President akichaguliwa aonyeshe mali gani akonayo ili tuje kujua sio mtu kwenda kufaidika pale na wananchi wana shida.Hicho ni kitu ambacho ningependa kuchangia.

Lile lingine ni habari ya makanisa. Mambo ya makanisa ningependelea iwe limited kwa sababu tukichunguza, inalipuka siku kwa siku.Tukichunguza ndani waanzishi wa makanisa ni wale ambao wamefukuzwa kwa kanisa zingine kwa maovu ambayo wametenda. Halafu kesho yake unasikia amekuja na hii. Serikali imefungua wazi kila mtu aombe mwenyezi Mungu lakini hata tunakuta hii devil worship wakaingilia hapo. Hii ningeomba Katiba ichunguzwe habari ya makanisa kwa sababu wengine wanahubiri mambo ambayo ni ya kustaajibisha.

Uone mtu ni ndugu ya huyu, na kwa hakika hawawezi kula sahani moja, hawawezi kwenda njia moja kwa sababu hii kanisa imeenda hivi. Hii imeenda hivi. Na hii ni kutawanya watu wa Kenya kupitia kwa makanisa hata sio mambo ya siasa. Hii makanisa imelete ugonjwa katika nchi hii, na ndio hata wengine wanasema ni kanisa unasikia wasichana watahirishwe ifanyike hivi, utakuta ni kama watu wa makanisa. Inginge hajulikani ni kanisa aina gani. Kwa hivyo, hii ichunguzwe na iwe imepunguzwa.

Hilo lingine ni juu ya vyama vya siasa. Vyama vya siasa kama KANU na hizo zingine. Zingepunguzwa ziwe kama vyama tatu, nne kwa sababu nchi hii ni moja tuu. Ili pawe na opposition ambayo iko na nguvu. Tuwe na chama kinachoshinda kiwe na nguvu kuzidi chochote. Tunaelewa ya kwamba, chama ambacho kitashinda kutakuwa na President, Vice President, Prime Minister kama katiba ya sasa ambayo itakumwa. Chama kitakacho shinda ndicho chama kitakachotoka Prime Minister. Chama kinashinda ili Prime Minister aunde serikali. Katika nchi zingine za nje, hakuna nchi zingine huchagua Prime Minister. President ambaye amechguliwa ndio anappoint Prime Minister kupitia chama. Ni bahati yetu katika Kenya tunatengeneza Katiba lakini tunataka tuwe na mweleko kwa sababu nchi nyingi zinatengeneza katiba lakini tunataka tuwe na mwelekeo kwa sababu nchi nyingi zinatengeneza katiba zikiwa na shida, lakini hii yetu tunatengeneza tukiwa katika hali safi. Hakuna vita. Nchi nyingi zinatengeneza katiba kukiwa na mapinduzi. Lakini hii yetu tunatengeneza tukiwa na katiba inatawala nchi hii haina shida. Kwa hivyo, tuwe na mwelekeo wa kujua tunarekebisha nini. Hicho ndicho kitu ambacho wengi hatuwezi kuwa tukielewa.

Jambo lingine ni habari ya elimu. Tukichunguza kwa makini tumekuwa na shida hapa na pale kwa sababu

mambo imechafuka kutoka upande ule, na ukiuliza hili unasikia inatoka juu. Kile kitu kinatoka vizuri ni kile kinatoka chini kinaenda juu. Kwa sababu hili limetoka juu, na ukifuata ni kitu fulani kimepitia kando tu, mvunguni wa meza inasemekana imetoka juu. Kwa hivyo, hilo tunaomba likomeshwe ili watoto wetu wawe katika mstari wa kusoma kwa sababu imekuwa corruption katika elimu. Ni mingi, sio moja au mbili au tatu. Na hiyo ni shida. Na watoto wamekuwa wakiangaika hapa na pale. Mimi sina mengi. Ni hayo tu, machache.

Com Aroni: Andrew Muindi. Mumo Kennedy, Lilliam Nyiengo Nzuni. Justine Kasinga.

Ms. Kasinga: Kwa majina ni Justine Mukami Kasinga. Yetu tumeandika, lakini niko na mbili au tatu nataka kutolea mkaza.

Moja ni juu ya citizenship. Ningeomba serikali yetu iwe na kiwagno fulani ya pesa ambayo watu wenye wameretire wawe wanapewa. Zile pesa wanapewa ziwe zinatoka kwa ile kodi tunalipa. Lngine ni kuwa, watu waliofikia umri wa 50 – 60 wawe pia wakipewa pesa kwa sababu hawana nguvu ya kujisaidia. Kuna mataifa ambayo watu waliozuka wanalindwa. Si mapendeleo ya Wakamba kuwa mtu aishi nao mpaka wakafa. Kwa hivyo ningesema serikali iwe inatoa pesa ya kulinda waliozeeka ambo wamekaa kwa hii nchi wakifanya kazi na hawajaenda popote.

Lngine ni juu ya tradition. Traditions, sana sana za Wakamba ziangaliwe. Zitaangaliwa vipi? Tuende kwa hili tunaita circumcision. Wakati watu walikuwa wakipitia circumcision, prostitution haikuwa juu kama wakati huu wa leo. Na wengine wenu wazee mnajua hiyo. Kwa hivyo, nasema traditions ziheshimiwe kabisa.

Lngine ni, wakati wazee walikuwa wanaenda kutoa sadaka kwa shrines. Hiyo kitu imekataliwa. Ni kama imeisha. Na imemaliziwa na wazungu. Wakasema tunaabudu shetani. Lakini hii haikuwa ya shetani. Kwa hivyo nasema sacrifices at the shrines should be practiced. That is under traditions.

Lile lngine ambayo iko under traditions ni marriages. Zamani watu hawakuwa wanaowa watu wa ukoo mmoja. Ikiwa ni ukoo wa Ambua, hawakuwa wakiowa Ambua wengine. Walikuwa wakiowa pengine Wakitondo au Amutei. Kwa hivyo, tradition ya marriages should be practised. Zingine zetu tumeandika, and my group and I will be very happy to see our views incorporated into the new Constitution. Asante.

Com Aroni: Before you go, we would like some clarification. Are you saying we should legalise Female Genital Mutilation (FGM)? Unataka turudishe na kuhalalisha hiyo tohara kwa wasichana, kwa sababu imetoa hiyo kama mfano.

Ms. Kasinga: Eeh! Juu sasa kwa wasichana Wakamba hiyo imeisha. Hata kama...

Com Aroni: What is the connection between prostitution na tohara kwa wasichana? What is the connection really? Nisaidie kuelewa kwa sababu nadhania tumeong'onezana hapa hatuelewei. Ina uhusiano gani?

Ms. Kasinga: Ni hivi. Ikiwa wasichana hawajapitia circumcision huwa influenced na prostitution.

Com Aroni: How? Eleza na kizungu.

Ms. Kasinga: Hapana. Sasa siwezi nikaeleza kwa kizungu vizuri.

Com Aroni: Asante. Joseph Mutungi

Mr. Mutungi: My names are Joseph Mule Mutungi and I am presenting a report on the group. However, our report is written, I will expand on several other important issues.

I will start with a preamble. The national vision which is to be set out in the preamble will include the national unity, peace, sovereignty or integrity of the State, security, justice, promotion of welfare and liberty or freedom. The common experiences of injustice to Kenyans to be reflected in the preamble should include inequality, discrimination, exploitation, corruption, poverty, diseases, unemployment, poor governance, lack of sufficient basic needs and suppression of human rights. Directing principles of state policy, the democratic principles to be included in the Constitution, the rule of law, recognition of human rights, good governance, equality and non-discrimination, devolution of power, reflection of the will of the people, promotion of justice and participatory governance.

Important values to be reflected include the building of a free society, unity and peace, recognition of the solidarity rights, socio-economic. Constitutional supremacy. Parliament should not have the sole power to amend any part of the Constitution. This can be done by the re-institution of the Senate and such that amendments are recommended after 65% of majority vote of both Houses. Requirements of some few months before the introduction to provide proper public facilities for discussion and reflection in case of a review. Some part of the Constitution should have restriction to be amended. They should require higher percentages majority votes in both Houses like 75%. Some other parts of the Constitution should be unamendable; the human rights.

Where amendment can be referred to the people, the public should be involved through referendums. Such referendums should be conducted by the legislature through Parliamentary Committee. Citizenship may be

acquired through birth. I won't explain much about citizenship by birth but I will talk about Kenyan citizenship acquired by naturalisation. This is the naturalisation of aliens or foreigners who have willingly adopted Kenya after satisfying the following qualifications: having lived in Kenya at least for the last ten years; a person who understands the rights and duties of a Kenyan citizen.

It should be granted to a person who can use Kenya's national languages, a person of impeccable character, a person who intends to continue living in Kenya, a person who has attained 18 years of age and above, a person who knows and understands the history, geography and government of Kenya. Such a person must give up citizenship in his or her motherland upon accepting citizenship, the person must accept the oath of allegiance in a court of law.

Com. Aroni: You are going to read the whole document?

Mr. Mutungi: No, I am not reading all. I am looking at the important ones. On defence and national security. The disciplined forces, the military, paramilitary, the police, prisons etc. should be established by the Constitution and that there should be mechanisms for disciplining such armed forces. The Parliament should have the power to define and punish pirates and fellow thieves and offences committed against the law of our country. The power to invoke emergency should be vested in the Prime Minister who also has to get affirmative action in effecting such emergency powers from Parliament.

Political parties should be co-operative and their Constitutions should be consistent with that of the State. Internal organisation of any political party should conform to the democratic principles and should not contravene the Constitution of the State.

Legislature; the central functions of Parliament should be expanded. These include; the power over the government taxing and spending. The Parliament should have power and veto over the budget proposals brought in by the Prime Minister and his cabinet. It should also entrench the power of reviewing its own members. Entrenchment of the office of the leader of the Opposition with enough resources to carry out functions of the opposition and to assist the other political parties.

Speaker: (Kikamba)

Translator: Namba sita ni juu ya kuabudu kanisani kwa sababu watu wote hawawezi enda kwa kanisa moja au dini moja kuna wengine pia hawaendi kanisani kama nchi yetu iko na uhuru. Kila mtu pale anaabudu hata kama ni kwa shrine aachwe aendelee kuabudu hapo. Nikawa na mambo sita mengine nimeandika.

Com. Aroni: Josiah Kituku, Zipporah, Jonathan, Allison, Esther Mweu, Monicah Mutua.

Ms. Mutua: Commissioners na watu wa Kilome. Mimi naitwa Monicah Ngina Mutua Kutoka (?) Location. Niko na machache kama manne hivi. Ya kwanza ni inheritance yaani utiwa. Naona wakina mama wazee huko wacha saa ingine mi sema hivi ile heritage inatakiwa iangaliwe na Commission hii ya sheria.

Kama ni mali mzee akiwa kama 60 hivi aite watoto wake agawanye kila kitu. Na akipeana asisahau yeye mwenyewe kama ni shamba na bibi yake maanake akigawa huenda watoto wake wakaharibu kila kitu kama vile tunasoma kwa bibilia na arudi na akute mzee na bibi hawana kitu.

Ile ingine naomba Commission iangalie ni widows na widowers na orphans. Kenya hii kuna wakina mama hata na wazee na watoto wengi sana. Kama ni mama akiachwa na bwana yake wale brother wa bwana wanamwingilia hata wengine wanaanza kusema hata naona sura hii ya huyu si wetu. Kwa hivyo mama you are to go kwenu. Kwa hivyo naonelea serikali iwe macho sana na ianzie hapa chini kwa villages na mama akiachwa, manager, assistant chief, chief waangalie. Na kuna widows wengine na widowers na orphans wale wanaachwa kama ni mama anaachwa na watoto wake mzee amekufa na ukimwi na tunajua mama hata yeye atakufa na pengine hawana mahali pa kukaa na ukiangalia Kenya hii kuna mashamba kubwa sana.

Mtu ameretire amekuwa ofisa wa serikali anapatiwa acres kama ishirini, 30, 40, 100 sasa ninaomba serikali na Commission hii ichukue hii maacre ipatie mtu huyo hana acre mingi apatiwe kumi na hizi zingine ipatiwe wale watu ambao hawana mahali ya kukaa maanake akiwa anasumbuka hata watoto ndio unaoona wananarandaranda, tunawaita wachokora. Si wachokora ni taabu imezidi. Na kama ni mzee naye aangaliwe. Asiwe kama ameachwa na bibi yake labda bibi ya brother yake ndiye amebaki huyu brother asiingilie huyu bibi labda amekufa na ukimwi, asipelekewe bibi yake naye ukimwi.

Na kama iko taabu fulani nayo serikali iwe inaangalia, watoto hivi. Ile ingine ni wale watoto wamesoma. Kuko na watoto wengi sana wametoka university na wako huku nyumbani na unaona mtu anakalia ile ofisi yake ama mahali, miaka nenda miaka rudi. Naomba hii Commission mtu akifikia tu miaka kama 60 ama 55 ile ilikuwa ya zamani atoke kwa hiyo ofisi na asiseme ati yule wao aandikwe hapo.

Wale watoto wamesoma wapatiwe preference waandikwe makazi. Na asiwe ati kuna wakati mwingine huu mtu akienda aitishwe rushwa. Serikali iangalie sana hii rushwa ya mtu akitafuta kazi anaitishwa pesa nyingi hata kama ni kwa armed forces ukituma mtoto huko akafanye interview anaitishwa Kshs.50,000 na hata ile fare alienda nayo huko tueseme Makueni ni ya kuomba. Mzazi alienda akakopa fare yake na kukuja kufika huko anaambiwa apeane Kshs.50,000, kama si Kshs.50,000 you are to go. Hiyo iangaliwe sana. Mtoto akimaliza shule aandikwe kwa ile kitu alisomea aandikwe huko ikiwezekana.

Ile ingine ni kama serikali imesema kitu ifanye. Wacha tuseme ati tunasikia kuko na sub-district na ukienda hapo Kilome unaambiwa enda huko Makueni uende ukachukue kitu yako ya title deed what what. Tunataka ikiwezekana serikali ikisema hapa ndio Enzai pawe Enzai, si ati panaitwa Enzai kimdomo na officially si Enzai. Maanake unasikia hata wengine unaona unasikia headquarters waende huko wakapatiwe shamba huko but wakifika huko wanapigwa. Sasa hata tunajiuliza serikali gani hii. Mtu anaambiwa mnatakikana mwende kule. Mkienda huko mnapigwa sasa hii hata saa ingine mnapelekwa huko kortini. Hii yote tunataka serikali ikisema kitu kifanywe kwa mwananchi kifanywe. Hata kama ni pesa inatoka mahali ipelekwe mahali fulani wale wengine wasiwe ati wanaeka kwa mfuko. Hiyo iende kwa huyo mwananchi kabisa.

Sasa ile ingine ni ile inaitwa tradition kama ni ya Wakamba. Naonelea hii circumcision na hata na ile ingine ya kuomba. Saa ingine na of course wanawake wasikuwe wakitahiri na of course ile hivyo naoppose hii iwe final. Asante.

Com. Kabira: Thank you very much mama Monicah. Is it correct? Okay. Na tunauliza kama Peter Kamuya ako. Peter Kamuya Okay.

Mr. Kamuya: Commissioners, siku ya leo ni siku muhimu sana. Yangu ni kusema kuhusu administration. Mambo matatu nne. Naitwa Peter Kamuya.

Sasa tungeomba serikali ama Katiba tuliyotengeza leo iseme maasistant Chief na Chief waajiriwe na wananchi kutoka mashinani. Hiyo ni moja.

Lile ya pili ni mashamba, kuna mashamba kubwa imetengwa katika Katiba tuliyo nayo. Miaka tisaini na tisa mtu akiwa na hiyo shamba. Ningeomba hiyo Katiba tuko nayo leo ipunguze hiyo miaka 99 iwe kama hamsini hivi. Tuko na watu wamemiliki shamba acre kama mautu kumi na kuna vijana ambao hawana acre moja. Tungeomba Katiba ambayo tuko nayo tupunguze hiyo miaka 99, turudishe kama hamsini ndio wengine wapate ingawa robo acre.

Lile lingine ni kuhusu kimila ya Kikamba na kiapo. Lile ya tatu, wazee wa vijiji wanafanya kazi nyingi na tungeonelea serikali yetu tukufu ingewalipa kwa vile wanatumikia wananchi tukufu.

Lile ingine, mimi niko na miaka 45. Katiba iliyoko naonelea hayo mambo tungeendelea kutengeneza hayo halafu mimi nasikia niko katika sheria ya nchi yetu. Rais Moi asiwe chini ya sheria ama President yeyote atakuja Kenya hii. Asante

Com. Kabira: Asante sana bwana Peter Kanga, Nahashon Mugela. Hayuko. Geoffrey Muindi, hayuko.

